

## Ni nini ICANN?

Ushirika wa Intaneti wa Majina na Namba Zilizo Awazishwa [Internet Corporation for Assigned Names and Numbers (ICANN)] ni shirika lisilokuwa la faida lililoundwa kimataifa, lenye jukumu la kuhakikisha kuweko kwa nafasi za anwani za Itifaki ya Intaneti (IP), kuweko kwa vitambulisho vya itifaki, usimamizi wa Mfumo wa Domaini ya Kiwango cha Juu cha aina ya rejareja (gTLD) na fumbo la nchi (ccTLD), na shughuli za usimamizi wa mfumo wa seva ya shina. Hapo awali, huduma hizi zilitkelezwa kulingana na kandarasi za Serikali ya Marekani na Halmashauri ya Namba zilizo Awazishwa katika Intaneti [Assigned za Intaneti Internet Assigned Numbers Authority (IANA)] pamoja na viungo vyengine. Kwa wakati huu ICANN inatimiza wajibu wa IANA.

Kwa ushirika huu wa kibinagsi-na-umma, ICANN imejitolea kudumisha usawa wa uendeshaji wa Intaneti; kustawisha mashindano; kufaulu kupata uwakilishi mpana wa jamii za kilimwengu za Intaneti; na katika kuandaa sera sambamba na jukumu kwa kupitia mifumo ya maelewano ya kutoka chini hadi juu.

## Ni nini Mfumo wa Majina ya Domeini?

Mfumo wa Majina ya Domeini (DNS) unawasaidia watumizi kupata mwelekeo katika Intaneti. Kila kompyuta katika Intaneti ina anwani yake ya kipekee inayojulikana kama "anwani IP" (anwani ya Itifaki ya Intaneti). Kwa kuwa anwani IP (ambazo ni mfululizo wa nambari) si rahisi kuzikumbuka, badala yake DNS huruhusu mfululizo wa herufi unaofahamika ("jina la domeini") utumike. Kwa hivyo badala ya kupiga taipu "192.0.34.65," unaweza kuandika [www.icann.org](http://www.icann.org).

Hali ya kuweza kupata matokeo yaliyotarajiwu kutoka mahala popote katika Intaneti kunajulikana kama "utatuzi wa kilimwengu (universal resolvability)". Hali bii ni baadhi ya Mfumo wa Majina ya Domeini (Domain Name System - DNS) ambayo inaifanya Intaneti kuwa rasilimali ya manufaa na ya kilimwengu jinsi iliyivo sasa. Bila ya haya, jina la domeini laweza kukuelekeza kwa maeneo tofauti katika Intaneti kwa hali tofauti. Kisa kama hiki chaweza tu kuleta bumbuazi.

DNS inatafsiri jina la domeini unaloandika kwa kupiga katika anwani IP inayoaafikiana nayo, na inakuunganisha na wavuti (website) unaohitaji. DNS pia inawezesha barua pepe zifanye kazi jinsi zinavyo stahili, ili barua pepe unayotuma imfikie aliyetarajiwu kuipata.

## Ni Lipi Jukumu la ICANN?

ICANN ina jukumu la kusawazisha usimamizi wa viungo vya kifundi vya DNS ili kuhakisha kwamba utatuzi wa kilimwengu ili wote wanoitumia Intaneti waweze kuzipata anwani zote zilizo sawa. Inayafanya haya kwa kuchunguza usambazaji wa vitambulisho vya kipekee vya kifundi vinavyotumika katika uendeshaji Intaneti, na utumiaji na wengine wa majina ya Domeini ya Kiwango cha Juu (kama vile .com, .info, na kadhalika).


Maswala mengine ya muhimu kwa wanoitumia Intaneti, kama vile kanuni za shughuli za kifedha, udhibiti wa yaliyomo katika Intaneti, barua pepe za maeleo ya kibashara zinazotumwa ghafla (spam), na ulinzi wa takwimu hayako katika upeo wa jukumu la ICANN ya usawazishaji wa kiufundi.

## ICANN inafanya kazi kwa namna gani?

Katika muundo wa ICANN, serikali na mashirika ya mikataba ya kimataifa zinafanya kazi pamoja na biashara, mashirika, na watu wenye utaalamu wanao husika katika kuunda na kudumisha Intaneti ya kilimwengu. Uendelezi na ukuzaji wa Intaneti unaoendelea unasababisha changamoto mpya katika kudumisha uthabiti. Wanapofanya kazi pamoja, washirika wa ICANN wanashughulikia maswala yanayo husu azimio la ICANN ya uratibu wa kiufundi. Ikiwa sambamba na kanuni kamili ya kujikosoa wenyeve katika uchumi wa teknolojia ya juu, ICANN huenda ikawa ndio mfano bora zaidi wa ushirikiano katи ya wawakilishi wa jumuiya ya Intaneti.

ICANN inaongozwa na Baraza la Wakurugenzi lenye mseto wa kimataifa linalo endesha mfumo wa uandalizi wa sera. Rais wa ICANN anaongoza kundi la kimataifa, linaloshughulika katika mabara matatu, ambalo linahakikisha kwamba ICANN inatekeleza jukumu lake la uendeshaji kwa jamii ya Intaneti.

Ikiwa imeundwa kuitikia mahitaji ya uchumi pamoja na teknolojia zinazo badilika kwa kasi, mfumo wa uandalizi wa sera iliyo huru, na kutekelezwa kwa wakati hupata chanzo chake katika Mashirika Waruzuku. Kamati za Ushauri zinazotokana na mashirika watumizi, na jamii za kiufundi zinashirkiana kikazi na Mashirika Waruzuku ili kubuni sera zinazostahili na zenye manufaa. Zaidi ya serikali themanini zinapeana usaidizi wa dhati kwa Baraza la Wakurugenzi kupitia ile Kamati ya Serikali ya Ushauri.



Baraza la ICANN limewashirikisha wananchi wa Australia, Brazil, Bulgaria, Canada, Uchina, Ufaransa, Ujeruman, Ghana, Japan, Kenya, Korea, Mexico, Ubolanzi, Ureno, Senegal, Uhispania, Uingereza, na Marekani